

Mwafrika 23/4/63

Frelimo yasimama

MWANDISHI

Rais wa Frelimo, Dr. Eduardo C. Mondlane ndiye Mwandishi wa kumbukumbu hii ndefu kuhusu Msumbiji ambayo inatolewa katika gazeti hili kwa vipande vipande hadi mwisho. Usikose kipande chochote ili ufahamu jinsi Mreno anavyofanya Msumbiji.

LEO, Bwana Eduardo Mondlane, akiendelea na masimulizi yake juu ya nchi yake ya Msumbiji, anaeleza jinsi Bwana Gwambe alivyokuja kuanzisha Udenamo nchini Tanganyika; na baadaye jinsi Frelimo, chama anachoonzoga, kilivyoundwa.

“Akiwa katika nchi ya Rhodesia, Bw. Gwambe alijiingiza katika Umoja wa wananchi wa Msumbiji, na halafu akakubali kufika Dar es Salaam ili kuonana na kuwashawishi wanachama wa Manu wapate kuwajua Umoja. Alipofika Dar es Salaam

mwaka 1959, Tanganyika ilikuwa inajitayarisha kwa uhuru. Alipowasili Dar es Salaam, Bwana Gwambe ahlakiwa vizuri sana na wanachama wa chama hicho.

“Baada ya muda, Manu ilialikwa kuhudhuria mkutano wa vyama vinavyopitana ukoloni wa Kireno huko Rabat. Kwa vile wengi wa wanachama wa Manu hawafahamu Kireno, wakaamua kutuma Bwana Gwambe akawakilishe chama hicho katika mkutano huo.

“Kwenye mkutano huo, Bwana Gwamba alitamka kuwa anawakilisha chama cha Udenamo; na baada ya kurudi Dar es Salaam, akanzisha tawi la chama hicho cha Udenamo.

“Kwa muda, Udenamo na Manu vilikuwa vyama viwili tu vya wananchi wa Msumbiji katika Afrika ya Mashariki. Lakini baadaye, mwananchi mwingine wa Msumbiji, Bartazar Chagong'a, Rais wa chama kingine cha wananchi wa Msumbiji katika nchi ya Malawi (Nyasaland) —

Mozambique National Independence Party, alikuja na kujiunga na wananchi wengine wa Msumbiji katika Afrika ya Mashariki.

“Kwa miaka mingi, Bw. Changong'a alikuwa akifanya kazi katika hospitali, lakini alilazimishwa kujiuzulu katika kazi hiyo kwa sababu ya siasa zake za utaiifa ambayo Serikali ya Kireno haikuweza kuvumilia.

“Mambo yalipokuwa yanamwendea vibaya, Bw. Changong'a alikimbia Msumbiji na akafanya maskani Malawi. Lakini kwa kuwa Serikali ya Kireno kwa wakati huo ilikuwa huru kumtia nguvuni mwananchi wa Msumbiji katika nchi hiyo, akahamia Tanganyika. Kutoka Tanganyika, Bw. Changong'a aliniandikia barua kuniomba nifike kusaidia kuunda umoja.

Mozambique Liberation Front, yaani Frelimo, iliundwa mjini Dar es Salaam mwezi Juni mwaka 1962. Frelimo ni Umoja wa wananchi wa Msumbiji, ni umoja wa vyama mbalimbali vinavyowakilisha jitihada ya wananchi wa Msumbiji katika vita vya kupigania uhuru wao kwa muda mfupi iwezekanavyo.